# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI 15 NOVEMBA 2024

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, JENIPHER INNOCENT NZOBE**

Kwa wiki inayoishia tarehe 15 Novemba 2024, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliongezeka kwa kiasi cha asilimia 28.98, kutoka TZS 1.09 bilioni hadi TZS 1.41 bilioni ingawa kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua kwa asilimia 26.73 kutoka hisa milioni 1.56 hadi hisa milioni 1.17.

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.87, kutoka TZS 18.54 trilioni hadi trilioni 18.38. Mtaji wa Soko la Ndani uliongezeka kwa asilimia 0.02, hadi TZS 12.29 trilioni hadi TZS 12. 30 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya MKOMBOZI na TWIGA CEMENT.

TBL imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 683.01 milioni, ambayo ni 48.50% ya mauzo yote ikifuatiwa na CRDB iliyorekodi TZS 619.67 milioni, sawa na asilimia 43.93 ya mauzo yote.

Kwa upande wa bei, TWIGA ilipanda kwa TZS 20 na MKOMBOZI ziliongezeka kwa TZS 20 wakati hisa za AFRIPRISE zikipungua bei kwa TZS 5. Hisa DSE zilishuka kwa TZS 20, MCB zilishuka kwa TZS 5, NICOL ikishuka TZS 10.

Wiki hii ilishuhudia hisa za TBL zikiongoza katika mauzo kwenye kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa ndani wakiendelea kutawala mauzo ya soko wakirekodi jumla ya TZS 1.41 bilioni. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki ijayo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 95 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili TZS 130.64 bilioni.

Mnada wa Hatifungani za muda mrefu namba 564 uliofanywa tarehe 13 Novemba 2024, ulivutia zabuni 1135 ambapo zabuni 1047 zilifaulu. Jumla ya fedha zilizopatikana ni TZS 367.10 bilioni huku bei ya wastani ya mafanikio ikiwa 101.1117%.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA NOVEMBA 1, 2024. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**